# USAWIRI WA MASUALA IBUKA KATIKA FASIHI YA WATOTO: MIFANO KUTOKA KENYA

**Dr. Pamela M.Y. Ngugi**
**Chuo Kikuu cha Kenyatta- Kenya**
**Idara ya Kiswahili**
**Ngugi.pamela@ku.ac.ke**

## Ikisiri

*Fasihi ni zao la wakati katika jamii; jinsi jamii inavyobadilika ndivyo fasihi inavobadilika ili iweze kuyamulika masuala mapya yanayoibuka katika jamii husika kama vile, haki za binadamu, usawa katika jamii, madawa ya kulevya na mengine mengi. Kwa kuzingatia dhana ya hadithi-matini, makala hii imelenga kubainisha jinsi masuala ibuka yanajitokeza katika fasihi ya Kiswahili kwa watoto kwa lengo la kubainisha nafasi ya matini haya kama chombo cha kujenga uelewa na ufahamu kuhusiana na masuala ya kijamii.. Makala yatarejelea baadhi ya hadithi zilizoandikwa na waandishi mbalimbali kutoka Kenya.*

## 1.0 Utangulizi

Fasihi ya watoto imetumika na waandishi mbalimbali kuathiri wasomaji walengwa ili waweze kufuata mielekeo na mienendo ambayo inakubalika katika jamii ( Pinsent, 2005). Uandishi wa maudhui yanayohusu masuala ibuka na namna yanavyojitokeza katika kazi za fasihi ya Kiswahili kwa watoto ulianza kujitokeza kwa wingi hasa katika miaka ya 2002. Masuala ibuka ni dhana inayotumiwa kwa maana ya maudhui yanayorejelea mambo ambayo yamezuka na yanawaathiri wanajamii moja kwa moja (Njogu, 2007; Karanja, 2008). Ni dhahiri kuwa waandishi wa fasihi hii walianza kupata motisha, mwamko na kariha ya kutunga masuala haya kutokana na dhana ya Haki za Watoto ambayo ilitambuliwa na kutiwa sahihi na viongozi wa Umoja wa Nchi Huru za Kiafrika katika mwaka wa 1989 katika mkutano wa 16 uliofanyika Monrovia ( Lloyd, 2010). Nchini Kenya, sheria ya kuwalinda watoto ilipitishwa mwaka wa 1991 ( *The Hansard 2001)*). Kariha hii inatokana na mwamko wa jamii za kimaitafa kuyazingatia matukio mbalimbali yanayoibuka katika jamii ya kisasa na jinsi yanavyowaathiri watoto.

Fasihi ni zao la wakati, na jinsi jamii inavyobadilika ndivyo fasihi inavobadilika katika jamii ili iweze kuyamulika masuala mapya yanayoibuka katika jamii. Kwa mujibu wa Senkoro (1982), mwandishi yeyote wa kazi ya fasihi hawezi kujiepusha na hali halisi inayomzunguka kwa vile ndiyo iliyomzaa na kumkuza. Ni kwa msingi huu ambapo Wizara ya Elimu katika mwaka 2002, kupitia kwa Taasisi ya Elimu nchini Kenya ilipendekeza ufundishaji wa masuala ibuka katika shule za msingi na hata sekondari. Vile vile taasisi hii ilipendekeza kwamba waandishi wa fasihi ya watoto wayajumuishe masuala-ibuka katika uandishi wao, (Ministry of Education, 2002).

Ukweli ni kwamba ulimwengu wa sasa umezua mahitaji mapya katika maisha ya binadamu hasa ya afya, mazingira, siasa, elimu na haki za binadamu ambayo hayawezi kupuuzwa hasa katika uandishi wa fasihi za kihalisia. Masuala ibuka yaliyopendekezwa kushughulikiwa katika silabasi mpya ni pamoja na UKIMWI, unajisi wa watoto, dhuluma dhidi ya watoto, ajira za watoto, utunzaji wa mazingira na dawa za kulevya.

Lengo la kuyaangazia masuala haya ni kumfanya mwanafunzi awe na ufahamu wa maisha na hali inayomzingira na pia aweze kukuza uhusiano wake na wanajamii (Njogu 2007). Pia ni katika kuuwezesha mfumo wa elimu kuwalea wanafunzi na kuwapevusha ili waweze kutangamana na jamii kwa njia bora zaidi. Changamoto zinazoikabili jamii zinahitaji kukabiliwa kwa kutumia mbinu mseto za ubunifu ili malengo ya elimu yaweze kutimizwa kupitia njia mbalimbali ikiwemo fasihi. Uandishi wa hadithi ni njia mojawapo ya kuwafahamisha na kuwaelemisha watoto kuhusu hali mbalimbali za maisha. Makala hii imelenga kubainisha jinsi masuala ibuka yanajitokeza katika fasihi ya Kiswahili kwa watoto. Makala itarejelea baadhi ya hadithi zilizoandikwa na waandishi mbalimbali kutoka Kenya. Hii ina maana kuwa waandishi wamejaribu kuwafikia walengwa wa kazi zao kupitia dhana ya hadithi-matini.

### 1.1 Dhana ya Hadithi- Matini

Katika lengo la kutaka kuwafahamisha watoto kuhusu makala ya Umoja wa Mataifa ya Haki za Watoto kwa njia iliyo sahili na wazi, Shirika la *Language Intervention Associates* la Nigeria lilianzisha mradi wa kuandika hadithi kwa watoto (Osakwe, 2005). Lengo la kutumia mbinu hii ya hadithi-matini lilikuwa ni kutaka kuwapa motisha watoto ili waweze kusoma na kupata habari na maarifa kuhusu haki za watoto. Waanzilishi wa mradi huu walichukulia kwamba kutumia hadithi kama njia ya kuwasilisha ujumbe kunaweza kuibua matokeo bora zaidi kwa msomaji. Kupitia usomaji wa hadithi- matini, watoto wanaweza kukuzwa kijamii na kibinafsi.

Katika hadithi-matini, taarifa halisi huwasilishwa kupitia hadithi kwa kulenga maudhui yanayotolewa (Osakwe, 2005). Hadithi hiyo hulenga katika kuyafanya matini hayo kuwa ya kuvutia kwa msomaji au msikilizaji. Hadithi kama hizi si za kiurejelezi au za kumfanya msomaji kuibuka na mahitimisho yake binafsi bali huwa ni za kiuelekezi na za kiuadilifu. Kwa mujibu wa Reading (2005), hadithi hiyo hufanya kazi kama kichocheo cha kumvutia msomaji kwa maudhui ya hadithi. Kimsingi, matini- hadithi zinahitaji kuwa rahisi kueleweka kwa watoto walengwa. Kulingana na Osakwe (keshatajwa), hadithi-matini hulenga katika kutoa maelekezo na maadili kwa wasomaji. Hivyo basi katika hadithi-matini, hadithi huwa ndicho chombo cha kutoa mafunzo.

Dhana ya hadithi-matini imejengeka kwenye msingi wa utamaduni wa Kiafrika. Katika jamii nyingi za Kiafrika, hadithi zilitumika na zingali zinatumika kama njia ya kutoa mafunzo kuhusu amali mbalimbali za jamii, mahitaji ya kijamii na tamaduni zilizopendekezwa katika jamii husika. Matumizi ya hadithi kama chombo cha kufunzia yameungwa mkono na wataalamu wengi wa elimu. Kwa mfano, Giddings (1990),

anasema kuwa ujumuishwaji wa hadithi katika kuwafunza watoto huibua maana kwa mtoto, hasa pale ambapo hadithi inayohusika ina rejelea hali thabiti katika maisha ya mtoto. Garvie (1990) anahoji kuwa, hadithi husaidia katika kuweka kwenye muktadha yale yanayofundishwa, na hivyo kuleta maana, kuvutia na hata kuwapa wasomaji motisha ya kutaka kujua zaidi. Kwa sababu hiyo, hadithi inaweza kutumika kama Kiini cha kufunzia (*Thematic Approach to Education*), ambao ni mkabala unaopendekezwa utumike katika elimu. Katika kuunga mkono maoni haya ya Garvie (keshatajwa), Achebe akinukuliwa na Ezenwa- Ohaeto (2003) anasema kuwa katika umbile la binadamu, kuna kitu ambacho humfanya binadamu kuitikia kwa hadithi kwa njia ya haraka sana. Kwa sababu ya hadithi kuwa kichochezi, basi ni jukumu la mwandishi kuweza kufikiria kila wakati kuhusu, ni jambo lipi analoweza kufanya ili sauti yake iweze kuwafikia wanajamii kwa njia ya haraka na ya kuvutia?

Kwa ujumla, tunaweza kudai kuwa hadithi-matini ni mbinu ambayo ni muhimu kwa sababu kupitia kwayo, ujumbe muhimu huweza kupitishwa kwa wanajamii wote wakiwamo watoto na vijana ambao mara nyingi huwa hawana motisha wa kusoma vitabu vilivyo na ujumbe kuhusiana na hali ya maisha kama vile, afya bora, haki za binadamu, mazingira na kadhalika. Pia ifahamike kwamba mwandishi wa kazi za kifasihi ni wakala wa mabadiliko ya jamii kupitia kazi zake za kifasihi (Bakize 2014). Muhimu ni kutambua kuwa watoto husoma hadithi kutokana na ule uwezo wa kujitambulisha na wahusika katika hadithi hizo. Matumizi ya hadithi ni mbinu ambayo imetumika katika jamii kwa muda mrefu kama njia ya kuhakikisha kuwa ujumbe unaotolewa unahifadhiwa na wanajamii.

### 1.3 Namna Masuala Ibuka Yanavyoshughulikiwa katika Fasihi ya Watoto

Fasihi ya watoto katika jamii yoyote ile hulenga katika kuwafahamisha mambo yanayotukia katika jamii. Kama tulivyoeleza awali, jinsi jamii inavyobadilika ndivyo maudhui katika fasihi hii yanavyobadilika ili kulandana na hali ya kijamii. Ukweli ni kwamba watoto wa siku hizi wameshuhudia matukio mengi katika jamii hivi kwamba matukio haya yamewaathirii wengi wao moja kwa moja au kwa viwango mbalimbali. Katika sehemu inayofuata, baadhi ya masuala-ibuka haya yamejadiliwa na kisha kubainisha namna yalivyoshughulikiwa na waandishi mbalimbali wa fasihi ya watoto. Kimsingi ni kwamba mengi ya masuala-ibuka yanayoshughulikiwa yameegemea kwenye dhana ya Haki za Watoto.

#### 1.3.1 Dhana ya Haki za Watoto

Mswada kuhusu Haki za Watoto ulipitishwa katika mkutano wa Umoja wa Mataifa uliofanyika Novemba, 20, 1989, na ukaanza kutekelezwa katika nchi mbalimbali ulimwenguni kuanzia miaka ya 1990 ( Ehlers na Frank 2008). Kwa mujibu wa mswada huu, nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa zinahitaji kuurejelea mswada huu kama sheria za kulinda maslahi ya watoto. Mswada huu umejengeka kwenye mihimili minne ambayo ni: Haki ya Kuendelea Kuishi; mihimili huu unahusika na haki za watoto kuzaliwa na kutunzwa ili waishe maisha bora na yenye afya ya kiwango cha juu,

waweze kupata huduma za afya kila inapohitajika. Mhihimili wa pili unahusu Haki ya Kukua, ambapo mtoto ana haki ya kupata elimu bora ili iweze kumjenga kimwili na kiakili; kumjenga mtoto kitabia, kiroho na kiumbo. Mhimili wa tatu unahusu Haki ya Kumkinga Mtoto kutokana na kufanya kazi za sulubu na zinazohatarisha maisha yake pamoja na zile zinazomzuia mtoto kwenda shule au hata kukwamiza ukuaji wake kimwili na kiroho, kumkinga dhidi ya dhuluma zozote zile, kumkinga kutokana na shughuli mbalimbali za kijamii na kitamaduni ambazo zitamwathiri mtoto, kumkinga kuhusishwa na ngono za mapema. Mhimili wa mwisho unahusu Ushiriki wa Mtoto, ambapo mtoto anahitaji kupewa nafasi ya kushiriki katika maamuzi yanayotolewa kuhusu maisha ya mtoto; aidha, watoto wapewe nafasi ya kutoa maoni yao kulingana na shughuli zinazowahusu (Taylor, 2009; Ngugi, 2015). Mihimili hii ndiyo imekuwa msingi wa kuibua maudhui mbalimbali kuhusiana na suala la haki za watoto.

### 1.4 Suala la Haki za Watoto katika Hadithi

Waandishi wengi wameshughulikia masuala haya kwa njia mbalimbali. Katika kujenga hoja hii, sehemu inayofuata itatumia mifano michache kutoka kwa fasihi ya watoto ili kuonesha jinsi masuala ibuka yanavyoshughulikiwa katika jamii.Ili kufikia lengo hili, uhakiki wa kimaudhui (*content analysis*) ulitumika katika kushughulikia kila hadithi.

#### 1.4.1 Hadithi ya *Mama wa Kambo*

*Mama wa Kambo* ni hadithi iliyoandikwa na Catherine Kisovi na kuchapishwa mwaka 2005. Hadithi hii inasimulia maisha ya mhusika Kalaa, ambaye mamake mzazi anapoaga dunia, babake anaoa mke mwingine. Kitete, ambaye ni mama-mlezi anamtendea Kalaa ukatili. Kalaa ananyimwa haki ya kucheza na mtoto mwenzake kwa kisingizio kuwa atamchafua. Kalaa anafanyishwa kazi nyingi kama kufua nguo zao na azianike kabla ya kupata kifungua kinywa, akiamshwa wakati wa jogoo la kwanza ili awaandalie Kitete na bintiye kifungua kinywa. Mbali na kupewa kazi ngumu za kufanya, alinyimwa mavazi mazuri akawa anavalia matambara. Vile vile hakupewa chakula cha kutosha na hakuruhusiwa kwenda shuleni. Hata hivyo, baada ya babake kutambua yale yanayotendeka kwa Kalaa, anamwokoa kutokana na hali hii.

Katika hadithi hii, mtoto anafahamishwa kuhusu maovu yanayotendewa watoto wenzao katika jamii kama vile kunyimwa haki ya kutunzwa, kulishwa, kuvishwa kusomeshwa na hata kunyimwa nafasi yakushiriki michezo na wenzake. Mwandishi anaonyesha ukweli uliopo kuwa watoto wengi katika jamii huishia kuwa mayatima kutokana na vifo vya ama mzazi mmoja au wazizi wote kupitia hali kama ugonjwa wa UKIMWI, vita, njaa na magonjwa mengine. Hadithi kama hii ambapo mhusika anaibuka kuwa mshindi huweza kuwapa watoto matumaini katika maisha. Muhimu katika hadithi hii ni kuwa, watoto wote wanahaki ya kupata elimu na wasitengwe kwa misingi ya kutokuwa na wazazi.

### 1.4.2 Hadithi ya "Mtoto wa Mama" katika *Ngano za Mfalme TapwaraTapwara*

Hadithi hii ya "Mtoto wa Mama" kutoka katika kusanyiko la *Ngano za Mfalme TapwaraTapwara* imeandikwa na Katama Mkangi na kuchapishwa mwaka 2005. Mhusika mkuu katika hadithi hii ni msichana kwa jina la Umazi. Umazi amezaliwa katika familia ya mzazi mmoja. Mwandishi anaonyesha jinsi watoto waliozaliwa katika familia za mzazi mmoja wanavyopuuzwa na wanajamii. Kwa mfano, Umazi anapuuzwa na walimu na watoto wenzake kwa sababu wazazi wake hawakuoana. Hata hivyo, silka ya Umazi inawavutia wanajamii na hivyo basi kukubalika katika jamii.

Suala la familia ya mzazi mmoja ni suala lililoibuka kutokana na mabadiliko ya kijamii ambapo kutokana na sababu mbalimbali, mzazi mmoja anajikuta akiwaelea watoto yeye peke yake. Hapo zamani, hali ya kuwa na mzazi mmoja haikukubaliwa na jamii na iwapo ingetokea, basi jamii iliweka mikakati ya kukabiliana na jambo hilo. Hata hivyo, siku hizi wana jamii wameanza kulegeza msimamo wao kuhusu hali hii kwani familia za mzazi mmoja zinaendelea kuongezeka. Katama Mkangi anaihakiki jamii kuhusu namna jamii hii inavyowachukulia wanawake wanaowalea watoto pekee yao. Mtazamo huu unatokana na dhanagande ambazo zimerithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kuhusiana na nafasi ya baba na mama katika familia ( Adams na wengine 2011). Ili kubadilisha mtazamo huu, mwandishi anawatumia baadhi ya wahusika wake kuonyesha umuhimu wa kukubali familia kama hizi katika jamii ya kisasa. Kwamba hakuna sababu yoyote ya kuwatenga watoto wanaotoka katika jamii kama hii. Pia, mwandishi anaonesha kuwa mhusika Umazi ni mwadilifu na anawaheshimu watu wengine. Hivyo basi, hadithi hii imetumika kama wakala wa kuipa jamii mwelekeo mzuri kuhusu mabadiliko yanayotokea katika jamii.

### 1.5 Suala-ibuka la UKIMWI na Hadithi ya Watoto

Tangu kugunduliwa kwa UKIMWI katika miaka ya 1980, mkabala ambao umechukuliwa na wanajamii wengi umekuwa ni wa kulaumu, kukashifu, kunyanyapaa na kuwabagua watu wenye virusi vya UKIMWI au wale wanaouhusiana nao (Kinara 2011). Vile vile, suala la UKIMWI lilizungumziwa kwa mkabala wa vitisho uliotamalaki mno hasa katika miaka ya 80, (Njogu 2007). Muhimu zaidi ni kwamba wanajamii wanaendelea kuhamasishwa kuhusu namna ya kukabiliana na maradhi haya, wakiwemo waandishi wa hadithi mbalimbali (Mutembei 2009). Kutokana na namna ambavyo watoto huathirika na kutokana na kuibuka kwa janga la UKIMWI, hadithi mbalimbali zimeandikwa kuhusu suala zima la UKIMWI na athari zake kwa wanajamii kwa njia ya kuwapa wanajamii mafunzo mbalimbali kuhusiana na janga hili.

### 1.5.1 Hadithi ya *Yalianza Kimchezomchezo*

*Yalianza Kimchezomchezo* ni hadithi iliyoandikwa na Angelina Mdari (2001). Hadithi hii ina wahusika wawili, Rita na Suzzy. Rita akiwa katika darasa la tatu, aliokota gazeti lenye picha za uozo lililokuwa limetupwa pipani na jirani yao. Mwanzoni aliogopa kuzitazama picha hizo. Lakini kadri alivyendelea kuzitazama alizizoea. Alianza kutafuta

magazeti na vitabu vyenye picha kama hizo. Pia alivutiwa na nyimbo zenye maneno yaliyoelezea mambo ya ngono. Rita alianza kwenda vilabuni akiwa na Rafikiye Sussy. Mwishowe, wote wanaambukizwa virusi vya UKIMWI baada ya kukosa nidhamu na kuanza kushiriki pombe na uasherati vilabuni.

Katika kuwasilisha suala hili, mwandishi anaanza kwa kuwaonesha watoto namna ambavyo mwanajamii anaweza kujikuta katika hali walimojipata Rita na Sussy. Mwandishi anatoa maelezo haya kwa lengo la kumwelekeza mtoto. Uelekezaji wa watoto kuhusu nidhamu unatokana na haja ya kutaka kuwalinda kutokana na mambo ambayo yanaweza kuwaathiri kifikra na hata kiafya. Ulindaji wa maslahi ya watoto ni kipengele ambacho kimezingatiwa katika mkataba wa Haki za Watoto (2001) unaosisitiza kuwa kila mtoto anastahili kulindwa ili kusitokee jambo lolote ambalo linaweza kuhatarisha maisha yake. Vile vile, hadithi hii inachangia katika kujenga tabia nzuri miongoni mwa watoto kwa mujibu wa mkataba wa Haki za Watoto na pamoja na kuwatahadharisha watoto kuhusu marafiki wanaoweza kuwapotosha maishani mwao.

### 1.5.2 Hadithi ya *Alipata Tuzo*

Hadithi hii ya *Alipata Tuzo* imeandikwa na Pamela Ngugi (2006). Katika hadithi hii, wazazi wa Neema wanafariki kutokana na virusi vya UKIMWI. Neema analelewa na Babu na Nyanyake. Babu na Nyanya wanamlea kwa njia inayostahiki kiasi kuwa Neema aliwachukulia kuwa ni wazazi waliomzaa hadi pale anapopata habari kamili kutoka kwa wanafunzi wenzake. Neema anachukuwa hatua ya kutaka kujua ukweli kutoka kwa babu yake. Naye babu yake anamfahamisha ukweli. Ukweli huu unamtia Neema wasiwasi kwa sababu anaanza kufikira kuwa hata yeye aliambukizwa virusi vya UKIMWI akiwa mtoto. Lakini babu yake anamfahamisha kuwa mamake Neema alichukua tahadhari ya kumkinga asiambukizwe virusi. Neema anayakubali maisha jinsi yalivyo na anatia bidii masomoni. Anaendeleza kipawa chake cha uandishi ambapo baadaye anapta Tuzo ya Uandishi na masomo yake yanagharimiwa na wafadhili.

Katika hadithi hii, mwandishi anaonyesha umuhimu wa wazazi kushiriki katika kutekeleza haki za watoto. Kwa mfano, mama yake Neema anahakikisha kuwa amezingatia ushauri wa daktari ili asimwambukize Neema virusi vya UKIMWI. Hivyo basi, anamkinga kiafya. Katika siku za hivi karibuni idadi ya watoto walioambukizwa virusi inaendelea kubainika shuleni (Njogu, 2007). Hali hii imesababisha watoto wengi kukosa kuhudhuria masomo kutokana na kudhoofika kiafya au hata kubaguliwa na watoto wengine shule. Mwandishi anawahimiza watoto walioathirika na ugonjwa wa UKIMWI kupitia kupoteza wazazi wao kuwa wasife moyo. Tunamwona Neema akikuza kipawa chake cha uandishi na mwishowe anapata mfadhili wa masomo yake. Mfadhili huyu anamwezesha Neema kuendelea na masomo na hatimaye kutimiza ndoto yake ya uandishi. Kazi hii inaonyesha pia umuhimu wa kulea vipaji vya watoto (Bakize 2014). Ni muhimu vipaji hivi vitunzwe na kulelewa na wazazi na wadau wengine wanaohusika

na watoto. Kupitia kwa masimulizi kama haya, watoto waneweza kupata tajriba, uelewa na pia wakaratibu maisha yao kutokana na masimulizi kama haya.

**1.6 Suala la Ulemavu**

Kwa muda mrefu walemavu wamekuwa wakitengwa na jamii kwa sababu mbalimbali za kitamaduni. Kutokana na imani potofu za kijamii, baadhi ya jamii huwachukulia walemavu kuwa viumbe tofauti na binadamu wa kawaida (Pinsent, 2005). Ulemavu waweza kuwa wa aina mbalimbali kama vile ulemavu wa kuona, kutembea, kutoweza kusoma na kusema na ulemevu wa kiakili (Mahenge, 2013).Katika miaka ya hivi karibuni, suala la usawiri wa wahusika walemavu limepewa kipaumbele katika fasihi kutokana na jinsi mtazamo wa walemavu katika jamii unavyowaathiri wanajamii hawa katika maisha ya utotoni na katika utu uzima. Fasihi ya watoto inaweza kutumika kama ajenti wa kubadilisha mielekeo hasi ya watoto iwapo wao wenyewe ni walemavu au la.

**1.6.1 Hadithi ya "Ulemavu" katika *Ngano zaMfalme TapwaraTapwara***

Hadithi hii ya "Ulemavu" kutoka katika kusanyiko la *Ngano za Mfalme TapwaraTapwara* imeandikwa na Katama Mkangi na kuchapishwa mwaka (2005). Mwandishi ameshughulikia suala la ulemavu akitumia kisa cha Mvulana Kea. Katika hadithi hii, Kea anatengwa na wenzake kutokana na ulemavu wake. Mbali na kutengwa, wenzake wanamghasi kwa kila njia kama vile kumkodolea macho, kumcheka, kumzomea na wakati mwingine kumpiga. Mwandishi ameonyesha namna ambavyo Kea anateswa na Kesi kwa kumvunjia mkongojo aliotumia kwa kutembea. Umazi ndiye anayemsaidia Kea kutokana na ukatili wa Kesi.

Mwandishi analenga kuwafunza watoto kuwa walemevu ni binadamu na wana haki zao, kwa hivyo wasidhulumiwe. Katika hadithi hii, mwandishi anafunza watoto kuwa kuna aina mbalimbali za walemavu kama vile ulemavu wa ubongo. Kwa mfano, inabainika kuwa Kesi ambaye anamdhulumu Kea ana ulemavu wa ubongo. Kesi anamlazimisha Kea amfanyie kazi ya shule. Kea anapokataa, ndipo Kesi anamvunjia mkongojo wake.

Watoto wanahitaji kufahamishwa kuwa walemavu wanastahili kuthaminiwa.Yeyote anayewadhulumu, anastahili kuchukuliwa hatua. Kesi anashtakiwa kwa mwalimu mkuu wa shule na unafiki wake unafichuliwa. Mwalimu mkuu anamtaka Kesi aombe msamaha hadharani, kwanza kwa wazazi wake kwa kuwaaibisha na pili kwa watoto wote shuleni kwa kuwakosea heshima. Kupitia hadithi hii, watoto wanafunzwa kuwa kitendo cha kuwadhulumu walemavu ni kinyume na maadili ya jamii. Katika kumwadhibu Kesi, mwandishi amefaulu kutimiza matarajio ya mtoto kuwa uovu unahitaji kuadhibiwa.

**1.6.2 Hadithi ya *Si Kupenda Kwake***

Katika hadithi ya *Si Kupenda Kwake*, ilichoandikwa na mwandishi Pamela Ngugi, (2003) Rael ni mvulana mdogo aliye na kigugumizi. Ulemavu huu unamfanya achekwe

na wanafunzi wenzake pale anapoambiwa na mwalimu ajitambulishe. Rael anashindwa kulitamka jina Lake. Hali hii inamfanya Rael kuona aibu sana na anahisi kutengwa na wenzake darasani. Lakini mwalimu wa darasa anaingilia na kukatakaza wanafunzi kumcheka Rael kwa kuwaambia kuwa Rael hakupenda kuwa kigugumizi. Baada ya hapo, mwalimu anamhimiza Rael kufanya mazoezi ya kuzungumza akiwa peke yake. Mwishowe anajitoa katika ulemavu huu pale ambapo anashiriki katika mashindano ya kuzungumza hadharani na kuibuka mshindi. Ushindi huu unabadilisha mtazamo wake mwenyewe kujihusu na pia kuhusu watoto wengine kama yeye na wale wingine wanaowadharau walemavu.

Mwandishi analenga kuwatia moyo watoto walemevu kuwa wakati mwingine ulemavu waweza kuwa ni wa muda iwapo mtu atabadilisha mwelekeo wake na kujinasua katika hali hiyo kutegemea bidii yake mwenyewe. Vile vile, mwandishi anawapa walimu jukumu la kuwasaidia watoto kama hawa kwamba wasife moyo, na papo hapo akawahimiza wale wasio walemavu wawakubali walemavu na wasiwatenge.

### 1.7 Utunzaji wa Mazingira kama Suala- ibuka

Fasihi ya watoto huweza kusawiri suala la mazingira kwa njia mbalimbali. Lengo lake ni kutaka kuonyesha nafasi ya mazingira katika maisha ya binadamu (Njogu 2007; Njama, 2007). Mazingira yanapokuwa mazuri, jamii huweza kuishi vyema bila madhara yoyote. Kutotunza mazingira vizuri husababisha madhara makubwa kwa binadamu kama vile Maradhi, njaa, ukosefu wa maji na ukosefu wa hewa nzuri. Kwa sababu hii waandishi wengi wameshughulikia vipengele mbalimbali vya mazingira kama vile, kuonyesha uhusiano uliopo kati ya binadamu na mazingira, au athari inayoletwa kutokana na uchafuzi wa mazingira au hata kuonyesha jamii zinazotunza mazingira yao zikifurahia mazingira safi. Hadithi nyingi kuhusiana na suala la mazingira na utunzaji wake zimelenga kuwahimiza watoto kama wahusika kuwa maajenti wa kuyatunza mazingira yao, (Kunze 2014). Katika kufanya hivi, wanadhihirisha heshima na tathmini yao kwa mazingira.

#### 1.7.1 Hadithi ya “Mchuuzi wa Matambara”

Katika hadithi hii iliyoandikwa na Were (2000), mhusika Shimanyula anamtembelea shangaziye mjini Nairobi wakati wa likizo. Anapata fursa ya kutembelea mtaa wa mabanda uliokuwa karibu na jiji hilo. Mwandishi anaeleza kuwa njia za pale mtaani zilikuwa na mitaro mikubwa iliyobeba uchafu wa kila aina. Uchafu huo ulikwama na kutoa uvundo wa kutisha. Shimanyula alishangaa kuona kuwa kando ya mitaro hiyo, vyakula vya kila aina vilipikwa na kuuzwa. Shimanyula alianza kufikiria jinsi ambavyo magonjwa ya kila aina yangeweza kulipuka katika sehemu kama hii.
Mwandishi katika hadithi hii anaonyesha hali ambapo wanajamii wameyachafua mazingira yao bila hata kujali matokeo yake. Kupitia mhusika Shimanyula

anawatahadharisha wanajamii kuhusu matokeo ya kuishi katika mazingira machafu kwa kuonyesha kuwa wanajamii hao wanahatarisha maisha yao.

### 1.7.2 Hadithi ya *Ujeuri wa Mbwa*

Hadithi ya *Ujeuri wa Mbwa* imeandikwa na Pamela Ngugi (2005). Hadithi hii inahusu wahusika wanyama, Paka na Mbwa. Wanyama hawa wanaishi pamoja kwa ushirikiano. Lakini tatizo ni kwamba hawajui kuvitumia viungo vyao vya mwili ili kujipatia riziki au kuyalinda mazingira yao. Panatokea mtu mmoja ambaye anawafunza kutumia sehemu zao za mwili kama vile mapua ya kunusia na kadhalika. Vilevile, wanyama hawa wanatakiwa kuhudhuria mafunzo ya namna ya kutunza mazingira yao. Lakini Mbwa na familia yake wanakataa kuhudhuria kwa madai kuwa mafunzo ya unusaji yanatosha. Paka wanafunzwa namna ya kutunza mazingira kwa kufunika vinyesi vyao na hata kuonyeshwa usafi wa kunawa kila siku. Kutokana na kuyazingatia mafunzo haya, familia ya paka inajitunza na hivyo kuepukana na maradhi ya kuhara waliyokuwa wana pata kila mara. Kwa upande mwingine, mbwa wanazidi kupata magojwa ya kuhara kwa kukataa kujifunza namna ya kutunza mazingira yao.

Utunzaji wa mazingira ni suala ambalo limewashughulikia wanajamii wengi kutoka mataifa mbalimbali. Kwa mfano, baada ya Warsha ya "Mabadiliko ya Hali ya Mazingira Ulimwengu," Mshindi wa Tuzo la *Nobel*, Hayati Wangari Maathai, alitoa pendekezo la kuhusisha somo la mazingira katika taasisi za elimu, hasa katika shule za msingi na sekondari (Mathai, 2006). Alihoji kuwa watoto wakifunzwa namna ya kuyatunza mazingira wakiwa wachanga, basi watayalinda mazingira wakiwa watu wazima. Maoni ya Mathai (keshatajwa), ni kuwa watoto wanaweza kuwa maajenti wa kutunza mazingira iwapo watapewa mafunzo katika uwanja wa Elimu ya Mazingira. Jambo ambalo litaleta natija na mabadiliko makubwa katika jamii. Kimsingi ni kwamba mazingira mabaya huathiri hali ya maisha ya kila binadamu kila uchao. Hivi sasa suala la utunzaji wa mazingira limepewa kipaumbele katika silabasi ya shule.

## Hitimisho

Katika makala hii, tulilenga kuonyesha nafasi ya matini-hadithi katika kuyamulika masuala-ibuka katika jamii hasa namna ambavyo masuala-ibuka yanavyoshughulikiwa katika fasihi ya watoto. Imebainika kuwa jamii ni malighafi ya kazi za fasihi na kazi hizi zina nafasi kubwa ya kuathiri watoto wasomaji kwa njia mbalimbali. Muhimu zaidi ni kuwa, fasihi inastahili kuipa jamii, hasa watoto, mustakabali mzuri wa maisha kwa mujibu wa mabadiliko yanayotokea katika jamii ya wakati huu.

## Marejeleo

Adams, M. na wengine (2011). "Invisible or Involved Fathers? A Content Analysis of Representations of Parenting in Young Children's Picturebooks in the UK." In: *Sex Roles* (2011) 65:259–270 DOI 10.1007/s11199-011-0011-8

Bakize, L. (2014). *Utangulizi wa Fasihi ya Watoto*. Dar es Salaam: Maccony Printing Press.

Ehlers, L. & Frank, C. (2008). "Child Participation in Africa." In: Nilesen, J.S. (ed) *Children's Rights in Africa: A legal Perspective*. Engliand: Ashgate Publishing House. 111-127.

Ezenwa- Ohaeto. (ed) (2003). *Chinua Achebe's 'Straight from the Heart.* Awka, Nigeria: The Stone Press Publishers.

Garvie, E. (1990). *Story as Vehicle: Teaching English to Young Children.* New York: Multilingual Matters.

Karanja, D.W. (2008). Usawiri wa Masuala-ibuka katika Hadithi za watoto. Tasnifu ya Uzamili.Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Kinara, G. (2012). Maudhui ya UKIMWI katika *Ua la Faraja* na *Kala Tufaha.* Tasnifu ya Uzamili.Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Kunze, P.C. (2014). "Winnie- the-Concervationist: Tuck Evalasting, Ecofeminism, and Children's Literature." In: *The Lion and the Unicorn,* Volume 38, Number 1, pp. 30-44 (Article).DOI: 10.1353/uni.2014.0001

Lloyd, A. (2010). "The African Regional System for the Protection of Children's Rights." In: Julia Sloth-Nielsen (mhr) *Children's Rights in Africa*: *A legal Perspective*. England: Ashgate Publishing Limited.33-52

Mahenge, E. (2013). "Msigano wa Majina ya 'Walemavu' katika Jamii ya Wazungumzaji Kiswahili: Mifano kutoka Tanzania." Katika: *Kioo cha Lugha*.Juz 11:79-87.

Mathai, W. (2006).*Unbowed: A Memoir*. U.S.A.: Knof Publishing Group.

Ministry of Education. (2002). *Ministry of Education and Technology: Primary School Education Syllabus*. Volume 1. Nairobi: Ministry of Education.

Mutembei, A.K. (2009). *UKIMWI katika Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: TATAKI.

Ngugi, P.M.Y. (2015). "Developmental Change and Paece Among Children in Kenya". In: *Chemchemi. International Journal of Humanities and Social Sciences*. Kenyatta University.52- 65.

Njama, A.H. (2007). "Elimu ya Mazingira." Katika *Kiswahili na Elimu Nchini Kenya*. Nairobi: Twaweza Communications. 61-67

Njogu, K. (Mhr.) (2007). "Ufundishaji wa Masuala-ibuka katika shule nchini Kenya," Katika *Kiswahili na Elimu Nchini Kenya*. Nairobi: Twaweza Communications. 11-23.

Osakwe, N.N. (2005). "Creative Writing for Social Change: Story- Texts for Children in Nigeria." In: Kate Parry (mhr) *Teaching Reading in African Schools*. Kampala. Fountain Publishers.Vol 1. 181 – 194.

Pinsent, P. (2005). "Language, Genres and Issues: the Socially Committed Novel." In: Kimberley Reynolds (ed) *Modern Children's Literature*. New York: Palgrive Macmillan. 191-208

Reading, G. (2005) "Creating Hope through Reading: A literature based Multicultural Experience for Young Learners, using the ancient traditional tale, Cinderella." In: Kate Parry (mhr) *Teaching Reading in African Schools*. Kampala: Fountain Publishers.Vol 1. 159-180.

The Republic of Kenya (2001). *The Hansard*. Nairobi: Government of Kenya Printers.

Senkoro, F. E. M. (1982). *Fasihi.*Dar es Salaam: Press and Publicity.

Taylor, A.S. (2009). “The UN Convention on the Rights of the Child: giving Children a Voice”. In: A. Lewis and Lindsay, G. (eds) *Researching Children’s Persperctives*. Berkshire: Open University Press. 21-33.

**Vitabu mahsusi vya watoto**

Mdari A. (2001). *Yalianza Kimchezomchezo*. Nairobi: Focus Publishers Limited.

Mkangi, K. (2003). *Ngano za Mfalme Tapwara Tapwara*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Kisovi, C. (2005).*Mama wa Kambo*.Nairobi: Phoenix Publishers.

Ngugi, P. (2006) *Alipata Tuzo.* Nairobi: Longhorn Publishers

Ngugi.P. (2001).*Si Kupenda Kwake*. Nairobi: Oxford University Press

Were, E. (2006).*Mchuuzi wa Matambara*. Nairobi: Focus Publishers Limited

*Kuhusu Mwandishi*

*Dr. Pamela Ngugi ni Mhadhiri Mwandamizi katika Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. Yeye pia ni mwandishi wa fasihi ya watoto. Pamela ameandika makala mbalimbali kuhusu fasihi ya watoto katika majarida mengi.*